# EE BABA MIKONONI MWAKO

**PD. RICHARD KIMBWI (LUSHOTO PARISH TANGA 13/11/2005**







2. Kwa sababu ya watesi wangu nimekuwa laumu, Naam, hasa kwa ji- rani zangu/
   Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu, walioniona njiani wali- nikimbia.

3. Nimesahauliwa kama mfu asiyekumbukwa, Nimekuwa kama chombo kili-chovunjika/
   Maana nimesikia masingizio ya wengi, Hofu ziko pande zote.

4. Lakini mimi nakutumaini wewe Bwana, Nimesema wewe ndiwe Mungu wangu/
   Nyakati zangu zimo mikononi mwako, Uniponye na adui zangu nao wanaoni-fuatia.

5. Umwangazie mtumishi wako kwa nuru ya uso wako, uniokoe kwa ajili ya fa-dhili zako/
   Iweni hodari mpige moyo konde, Ninyi nyote mnaom-ngoja Bwana.

©